# KITU KIKUBWA SANA KATIKA MAISHA NI KUMKABIDHI MUNGU KITU FULANI

*Zaburi: 37:5, Umkabidhi Bwana njia yako pia umtumaini naye atafanya*

Hapa ndipo udhaifu wa wale waitwao wakristo wanaposhiidwa kupokea uponyaji (ile ahadi ) leo. Wanaangalia ile taa badala ya kuangalia kile Mungu alichosema. Ungewazia vipi mkulima akipanda mahindi yake naye aende kila siku na kuyafukua yote nje, aone kama yataenda kuota au la? Hataweza kupata mahindi. Yeye anayakabidhi kwa ardhi (udongo), chini ya wazo hili kwamba Mungu ameahidi hilo linamaliza kila kitu.

Hiyo namna tunayopata kila neno la Mungu, sababu ni mbegu na tunaipokea ndani ya mioyo yetu (Rumi 10:10) na kuikabidhi hiyo kwa Mungu na kusahau juu ya hilo. Mungu hamalizi yote yaliyobaki kwasababu ameahidi angefanya hiyvo. Neno la Mungu. Na kila Neno litazaa hasa vile lilivyo, kwasababu Neno ni mbegu.

Unaweza ukamchukua anayeonekana kama Mkristo, anatenda kama mkristo, lakini kama huyu mtu hana Neno la Mungu ndano yeke, kama hakuna chembe ya uhai pale il kuitia uhai, hawezi akafufuka kwenye ufufuo. Hiyo ni kweli. Kwasababu hawezi akafufuka; hakuna kitu pale cha kufanya afufuke tena: mbegu (Luka 8:1).

Sasa unapozika mbegu ili wakulima, unachukua na unaenda nje pale na kupanda mahindi yako, huendi kila asubuhi na kuifukua hiyo mbegu “hebu tuone sasa, inaota? Kitu chochote kimetokea hapana”. Unairudisha tena udongoni siku inayofuata jioni, unasema “natoka nione kama inaendelea vyema” unichimbua tena; haitaweza kamwe kuota kwa namna hiyo. Vema, jambo unalofanya na hiyo mbegu, unaikabidhi kwenye udongo, unaifukia; hivyo ndivyo uwezavyo juu ya hilo. Ni juu ya Mungu kufanya yaliyobaikia.

Vyema, hivyo ndivyo ilivyo neno la Mungu. Kama utachukua ahadi yoyote ya Mungu aliyeifanya biblia ukaiweka moyoni na kuinywesha kila siku na sifa za Mungu (Zaburi 34: 1), hiyo intaenda kutimia, itaota kama, kama hautaenda kuichezea hiyo, kama utaicha peke yake. Usiseme, “Ngoja nione, na weza kusogeza kidole changu vizuri leo, je nanajisikia vizuri, je maumivu ya kichwa yamekuwa nafuu sasa?” Oh! Hapana, haitakuwa hovyo kamwe, iweke mikononi mwa Mungu, na uendelee kwenda, na uliache lenyewe (Neno). Hiyo ni mbegu ya Mungu. Itaota (Marko 4:26-28) .

Lakini unajua mara nyingi hatujui Mungu hutenda kazi kwa namna ya kisiri jinsi ilivyo miujiza ya utendaji. Kama tunalikabidhi jambo lolote kwa Mungu na kuliamini, kama watoto wetu au chochote kiwacho, na tunaamini kwamba Mungu atajibu haya maombi. Likabidhi tu kwa Mungu. Hilo ndilo likupasalo kufanya. Na usiweke mkono wako tena katika hilo. Muache Mungu alishughulikie. Kama utaenda jambo fulani juu ya hilo, hapo basi atasimama nyuma na kuacha wewe uwendalee mbele mpaka uwe umemaliza. Lakini unapo likabidhi kwa bwana na kuamwacha alishughulikie, hapo sasa yeye atalifanya. Wewe unapaswa tu kumwamini yeye. Kaa nyuma tu,. Na usitende chochote, ili uamini. Hapo ndipo neema inapohesabiwa kuwa haki kama unaamini kwamba Mungu atatenda (Warumi 4:5).

Nisikilizeni mimi. Ninaenda kuzumgumza kitu kikubwa. Kila mara unapoangalia dalili zako, unachelewesha uponyaji wako. Usijaribu kuifukua tena. Imekabidhiwa kwa yeye aliyeahidi uponyaji yeye awaponyaye wote (Hesabu 21:4-9).

Unapopita katika mstari wa maombi na ukawekewa mikono juu yako. Biblia ilisema “maombi ya imani yatamponya mgonjwa” (Yakobo 5:15) usiseme vema, hebu tuone kama naweza kujisikia vizuri, moyo wangu unanafuu kidogo, mikono yangu ......... usifanye hivyo. Unachelewesha (uponyaji). Ukabidhi kwenye udongo kwa sababu ni mbegu.

Hapo sasa ni juu ya udogo kufanya yaliyo salia. Na kila mara unapoangalia dalili zako, unapozishuhudia, unapolalamika juu ya hizo Mungu hawezi kamwe kukuponya wewe mkabidhi Mungu na uamini Neno lake (1 Petro 5:7).

, tumbo la uzazi la moyo lililotakaswa kupikea Neno. Jalia hiulo, Bwana nawaweka kwako wewe uwachukue kutoka hapa, kama ikiwezekana hilo mmoja awe bibi arusi katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

***Nukuu za Kingereza***

*"Uhai ndio uponyaji" (57 – 0611), aya 038 – 039 "Tuonyeshe Baba na itatutosha" (60-0931), aya 044"Ee Mwana wa Daudi Nihurumie mimi "(61-0215), aya 016 "Tuonyeshe Baba" (62-0722) aya 051 "Hukumu ya mahakama" (64-0412) aya 038 "Bwana tunatoka kumwona Yesu" (62-0724), AYA 054 Dunia inaporomoka tena 63-1127, kitabu 17 na 4), aya 77 Umoja wa Mungu mmoja katika kanisa moja" (58-1221E kitabu 16 na 8) aya 153 "Kuishindania imoni kwa bidii" (53-0614A), aya 077 Neno lililonenwa ndiyo Mbegu ya asili (62-0318E) uk.129 aya 206*

---

Jiwe la kujengea la kiroho na 95 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii. Imekusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69; D-75328 Schomberge Germany Phone (+49) 72357613, Fax (+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao utakuwa ni Bibilia moja kwa moja na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu uliyokusudiwa kimbele imesikia.

Ndugu Branham katika Mwenendo na utaratibu na mafundisho Uk. 724

*Box 553 Korogwe – Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*